**Mpango wa Tuzo za Bolt ni nini?**

1. Mpango wa Tuzo za Bolt (“**Mpango**”) ni mpango kwa ajili ya taasisi zinazotoa huduma ya usafirishaji au madereva wanaofanya kwa niaba ya taasisi zinazotoa huduma ya usafirishaji kupitia jukwaa la Bolt au *Bolt Platform*. Mpango huu unakuwezesha kukusanya pointi za Bolt ili kuweza kufikia ngazi fulani za Tuzo za Bolt (“**Ngazi**”). Kama uko kwenye Ngazi husika ya Tuzo ya Bolt, basi unaweza kupewa aina fulani ya Tuzo za Bolt (“**Tuzo**”) ambazo unaweza kunufaika nazo endapo utakuwa katika ngazi husika.
2. Mpango huu unaletwa kwako na Bolt Operations OÜ, kampuni binafsi iliyosajiliwa chini ya Sheria za Jamhuri ya Estonia na kupata namba za usajili 14532901, yenye ofisi ya usajili nambari Vana-Louna tn 15, Tallinn 10134, Jamhuri ya Estonia, au kampuni nyingine iliyopo kwenye Kundi la Makampuni ya Bolt.
3. Masharti ya Mpango huu (“Masharti”) yamewekwa ikiwa ni ziada ya vigezo vilivyokuwepo tangu awali lakini pia ni kwa mujibu wa Vigezo na Sera za Faragha kwa Madereva, na kanuni hizi zinafafanua masharti ya kushiriki kwenye Mpango huu. Maneno yote yaliyo katika herufi kubwa yatakuwa na maana sawa ile iliyowekwa kwenye Vigezo na Masharti kwa Madereva.
4. Wakati programu ya Bolt, (Bolt App) inapotumika, Bolt inasimama kama mtoaji wa taarifa za huduma kwa jamii na si mtoa huduma ya usafirishaji. Manufaa yanayotolewa na Mpango huu yanatolewa katika misingi ya “as is basis” yaani Bolt haitawajibika kwa mambo ambayo hayakufahamika na Bolt wakati wa matumizi ya huduma hii na Pointi za Bolt zinatolewa kwako kwa kutegemea maombi ya huduma ya usafiri kutoka kwa abiria kupitia Mpango huu.

**Namna ya kushiriki kwenye Mpango huu**

1. Utakidhi vigezo vya kushiriki katika Mpango huu endapo;
a. Mpango huu upo na unafanya kazi katika mji uliopo,
b. Una akaunti ya Dereva ya Bolt na umefuata taratibu na kanuni zote za sheria zinazohusika kwa watoa huduma ya usafirishaji,
c. Kama mpango huu unatumika katika mji wako, kwa kiwango kinachokubalika na alama atakazopata dereva zifikie walau ngazi uliyowekewa kupitia programu ya Bolt (Bolt App).
2. Endapo dereva atakidhi vigezo vilivyoelezwa katika kifungu Na. 5 hapo juu, ataingizwa moja kwa moja kwenye Mpango huu.

**Yapi ni masharti ya Mpango huu?**

Pointi za Bolt

Kila safari inayofanyika kupitia jukwaa la Bolt inakupatia kiasi fulani cha pointi za Bolt kama zilivyoainishwa kwenye programu ya Bolt (Bolt App). Tambua ya kuwa kiasi cha pointi za Bolt kinachopatikana kwa kila safari kinatofautiana, kulingana na wakati wa siku unayotoa huduma ya usafirishaji kwa kupitia jukwaa la Bolt. Una fursa ya kupata pointi za Bolt zaidi wakati wa saa zenye foleni kubwa zaidi za magari. Muda wa foleni kubwa unaweza kutofautiana kwa kila mwezi. Saa zenye foleni kubwa katika mji wako zimeainishwa katika programu ya Bolt.

1. Utapata pointi za Bolt kwa kila safari inayokamilika kupitia programu ya Bolt. Hautapata pointi za Bolt kama haukukamilisha safari. Dhumuni la pointi za Bolt ni kuamua Ngazi yako. Pointi za Bolt haziwezi kuhamishwa na hazibadilishwi kwa fedha taslimu. Bolt ina haki ya kubatilisha hatua zako muda wowote endapo kutakua na viashiria vya tabia za ulaghai, matumizi mabaya ya jukwaa la Bolt (Bolt Platform) au kutofuata Kanuni hizi au Vigezo na Masharti ya Madereva.
2. Kulingana na kiasi cha pointi za Bolt unazopata kila mwezi wakati unapotoa huduma ya usafirishaji kupitia jukwaa la Bolt, utapangiwa Ngazi fulani katika Mpango huu. Zifuatazo ni Ngazi zinazotolewa katika Mpango huu

a. Ngazi ya Shaba
b. Ngazi ya Fedha
c. Ngazi ya Dhahabu
d. Ngazi ya Platinamu
3. Pointi za Bolt zinazotakiwa kuamua Ngazi yako zimeainishwa katika programu ya Bolt na zinaweza kubadilika. Utapewa taarifa za mabadiliko yoyote katika siku ya kwanza ya mwezi.
4. Kiasi cha pointi za Bolt kilichokusanywa kitafika ukomo wake na kitabadilika kuwa sifuri mwisho wa kila mwezi. Pointi zako za Bolt hazitahamishwa kwenda mwezi unaofuata. Ngazi hizi si za kudumu, kila mwezi deriva atafikia ngazi husika kutegemeana na pointi atakazokusanya kwa mwezi huo.
5. Ikitokea hitilafu yoyote ya kiufundi katika programu ya Bolt au mfumo wowote unaokuwezesha kutumia programu ya Bolt, pointi zako za Bolt zinaweza kuchelewa kuonekana katika programu yako ya Bolt. Bolt haitoi dhamana kuwa itakuwa na uwezo wa kurudisha pointi zako za Bolt zilizopotea kutokana na hitilafu ya kiufundi iliyotokea katika programu ya Bolt au mfumo wake lakini timu yetu ya usaidizi itafanya kila liwezekanalo kurudisha pointi za Bolt pale hali hiyo itakapojitokeza.

**Tuzo za Bolt**
1. Tuzo ni marupurupu yanayotolewa kwako. Tuzo zinatolewa kwa uamuzi binafsi wa Bolt na zinaweza kubadilika au kufutwa muda wowote, haziwezi kukombolewa kwa mbadala wa pointi za Bolt na haziwezi kuthaminishwa kwa fedha taslimu. Taarifa za kina kuhusu Tuzo hizo na vigezo na masharti yake zinapatikana katika programu yako ya Bolt. Kwa Tuzo zinazotolewa na mhusika asiyekuwa Bolt, unaweza kuhitajika kuchukua hatua zaidi ya zilizoelezwa katika masharti haya ikiwemo kutakiwa kukubaliana na vigezo na masharti ya ziada au kufungua akaunti na mbia au mhusika mwingine atakayekuwa anatoa Tuzo hizo. Pia katika mazingira fulani fulani, Bolt itashirikisha tarifa zako kwa wahusika wengine kusudi uweze kuzifaidi Tuzo husika. Bolt haina uwezo wa kudhibiti wahusika wengine katika matumizi ya tarifa zako binafsi. Matumizi yao ya tarifa zako binafsi yatakuwa kwa mujibu wa sera zao kuhusiana na sera zao za faragha.
2. Pale utakapokuwa umepata pointi za Bolt zinazohitajika kwa Ngazi fulani, kama inavyoonyeshwa kwenye programu ya Bolt, moja kwa moja utapata Tuzo zinazotolewa katika Ngazi uliyoipata. Tuzo zinazotolewa katika kila Ngazi husika zimeainishwa katika programu ya Bolt.
3. Tuzo zinazotolewa ndani ya Mpango huu zinaweza kutolewa na Bolt au mhusika wa mwingine asiye Bolt. Bolt haiwajibiki kuhakikisha kuwa unapata Tuzo zinazotolewa na mhusika mwingine hata kama unastahili Tuzo hiyo kwa mujibu wa vigezo na masharti haya pale ambapo sababu za wewe kushindwa kuipata tuzo hiyo ziko nje ya uwezo wa Bolt.
4. Una wajibika na kodi zote za serikali zinazoweza kuwepo kutokana na wewe kupewa Tuzo huzika.

**Masharti mengineyo**
1. Endapo vigezo vya wewe kuingia katika Mpango huu vimepitishwa na Jukwaa la Bolt, unaweza kusimamishwa kwa muda katika Mpango huu hadi pale utakapo pata tena kiwango kinachokubalika na alama za dereva zinazohitajika kuweza kushiriki katika Mpango huu. Kusimamishwa katika Mpango huu inamaanisha kuwa unapoteza uwezo wa kupata Tuzo ulizojishindia na kupoteza haki ya kupata pointi za Bolt kwa safari utakazofanya katika kipindi ulichosimamishwa. Kiwango kinachokubalika na alama za dereva zinazohitajika kushiriki katika Mpango huu vimeainishwa katika programu ya Bolt.

2. Bolt inaweza kusitisha, kusimamisha au kubatilisha ushiriki wako kwenye Mpango huu muda wowote kwa kukupa taarifa kabla. Kama ushiriki wako kwenye Programu umesitishwa, pointi za Bolt ulizojikusanyia zitafutwa na hutaweza kuzitumia tena endapo utajiunga tena na Mpango huu. Kama Bolt itabaini ulaghai au ukiukwaji wa vigezo na masharti ya Mpango huu, ushiriki wako kwenye Mpango huu utasitishwa au kusimamishwa au utabatilishwa mara moja. Ikitokea vitendo vya ulaghai au ukiukwaji wa vigezo hivi umegundulika, mbali na kunyang'anywa pointi zote za Bolt, utanyimwa kabisa haki ya kujiunga tena na Mpango huu.

**Mwisho**

1. Unapaswa kutambua kuwa Bolt inaweza kusitisha au kurekebisha Mpango huu au sehemu yoyote ya Mpango huu katika muda wowote kwa kadiri Bolt itakavyoona inafaa. Maamuzi ya kusitisha au kurekepisha Mpango huu ni pamoja na mabadiliko katika Tuzo zinazotolewa katika Mpango huu, Pointi za Bolt zinazohitajika kufikia Ngazi Fulani, mpangilio wa Ngazi, vigezo vya kufikia Ngazi Fulani na muda wa Mpango huu. Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo Bolt inaweza kurekebisha kadiri inavyoona inafaa au kuondoa kabisa.
2. Haki na wajibu wa Bolt katika Mpango huu zinaweza kupewa au kuhamishwa na Bolt kwa mtu au taasisi nyingine yoyote iwe ina uhusiano na Bolt au haina uhusiano wakati wowote. Baada ya mabadiliko ya uhamishaji wa haki na wajibu kutoka Bolt Kwenda kwa mhusika mwingine, utekelezaji wa Mpango huu utakuwa ni wajibu wa mhusika huyo aliyechukua haki na wajibu wa Bolt.
3. Mpango huu au kipengele chochote cha Mpango huu kinaweza kikashindwa kupatikana au kupatikana bila usahihi unaotakiwa au kuwa na muingiliano katika nyakati fulani fulani kutokana na sababu tofauti zilizo nje ya uwezo wa Bolt. Bolt haitawajibika kwa kutokupatikana kwa Mpango huu au kwa muingiliano, au makosa yanayoweza kutokea katika Mpango huu au kwenye sehemu ya mpango huu (features) wakati wowote na bila taarifa. Bolt inaweza kurekebisha, kuzuia au kusimamisha Mpango huu au kipengele chochote muda wowote bila kutoa taarifa.

Bolt, washirika wa Bolt au mhusika mwingine anayetoa Tuzo na mawakala wao hawatoi hakikisho lolote iwe waziwazi au kwa namna isiyo ya waziwazi kuhusu usahihi, sarafu/fedha, ukamilifu wa Mpango huu, utendaji kazi wa Mpango huu, taarifa, nyenzo, maudhui, upatikanaji, na bidhaa au jambo jingine lolote ambalo halijatajwa hapa. Kwa namna ambavyo sheria husika inaruhusu, Bolt inaweka angalizo kwamba haitoi dhamana yoyote iwe waziwazi au vingineyo ikiwemo dhamana ya biashara au dhamana ya kuwa malengo tarajiwa yatafikiwa au jambo linguine lolote lililo nje ya uwezo wa Bolt kudhibiti.